

ASb  
approved



# Anansi mlafi


Ursula Nafula  
Wiehan de Jager

Kiswahili



Anansi aliwakuta  
kunguru wakila  
makuyu.

Yeye pia alitaka  
makuyu.



Kunguru  
walimpatia Anansi  
makuyu.



Kunguru  
walimwambia,  
"Sasa njoo uchume  
makuyu nasi."



Walienda kuchuma makuyu pamoja.

Lakini Anansi alichukua makuyu yote.



Anansi aliruka.

Alianguka ndani ya  
mto uliojaa  
mamba.



Anansi alisema,  
"Mimi ni mmoja wa  
jamaa zenu."

Hakuliwa.




Anansi alijifanya  
kuwa anakunywa  
maji chafu kama  
mamba.






Mamba  
walimwamini  
Anansi.

Walimualika kukaa  
nao.



Anansi alisema,  
"Nitakaa, lakini,  
hebu kwanza  
niilete familia  
yangu."



Mamba alimbeba  
Anansi hadi ukingo  
wa mto.



Anansi alitoroka.

Mamba bado  
anamsubiri hadi  
leo.

## Anansi mlafi

**Author** - Ghanaian folktale  
**Translation** - Ursula Nafula  
**Illustration** - Wiehan de Jager  
**Language** - Kiswahili  
**Level** - First words

© African Storybook Initiative 2014  
Creative Commons: Attribution 4.0  
Source [www.africanstorybook.org](http://www.africanstorybook.org)